

**Swahili transcript:**

Happy: Kanga mara nyingine inatumika katika kujifunika. Kwa mfano unapoenda msibani, mara nyingi unakuwa wanawake wamevaa kanga na nyingine wanajifunika kama hivi. Inatumika..mara nyingi ukienda msibani unakuta wanawake wamevaa kanga wamejifunika kama hivi. Au saa nyingine mtu anapokuwa anataka kwenda sokoni, ana haraka zake, labda amevaa tu kanga moja, labda anataka kwenda nje labda amevaa tu kishati, halafu mtu mwingine hapendi kutembea labda akiwa yuko waziwazi, anaweza tu akachukua kanga, akajifunika juu na akaendelea na shughuli zake. Akajifunika tu hivi, akaendelea na shughuli zake. Kwa hiyo, kwa kifupi, hilo ndilo vazi la kanga. Na pia kanga, inatumika katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano, unapokuwa na mtoto, unapokuwa unambeba mtoto, kanga inakuwa inatumika. Na mara nyingi kubebeba mtoto, kanga inakuwa inatumika; mfano ukimweka mtoto wako mgongoni, halafu hii inakuja hapa. Unakuwa umemweka mtoto huku, mtoto anakuwa kwa huku, halafu unafunga hivi. Kwa hiyo, unaonekana umebeba mtoto wako kwa hapa, anakuwa amekaa hapa, miguu inaning'inia huku na unakuwa umemfunga vizuri na kanga. Pia, kanga inaweza ikatumika katika kujifunga kwa mfano kichwani. Kwa mfano mimi hapa si nimefunga tu kitambaa hivi; lakini kanga mara nyingine inatumika katika kujifunga kichwani. Kwa mfano mabibi harusi kwenye kitchen parties wanakuwaga wanavalishwa kanga. Kwa hiyo mtu anaweza akajifunga labda hivi, halafu aka..ukatengeneza ua lolote unalotaka. Unaweza ukatengeneza likawa hivi. Aaah! Hii tu ni simple, lakini kuna wengine ambao wakitengeneza wanaweza wakatengeneza na maua, au hii ikakaa upande huu, au ikakaa nyuma, au ikakaa hapa mbele halafu ukaitengenmeza vizuri. Lakini hii tu ni mfano. Na pia saa nyingine kanga inatumika katika kupambia maharusi; au tu kitu chochote kile katika nyumba. Unaweza ukakuta kanga wametengeneza kama hivi, halafu hapa katikati labda wanakuwa wame..wamefunga. Wameifunga hivi. Halafu wanakuwa wanatengeneza kitu kama kipepeo, inakuwa yaani kama butterfly hivi, halafu wanakuwa wanaitundika labda ukutani kama hivi. Kwa hiyo, inakuwa inatumika kama mapambo katika shughuli mbalimbali, labda harusi, kitchen party, au kipaimara. Hii inakuwa kama

umbo hili, inakuwa kama kipepeo, inakuwa kama hivi. Imekaa kama butterfly kidogo; ila huu tu ni mfano. Ukitengeneza vizuri katika ukuta inakuwa inapendeza zaidi

**English translation:**

Happy: In other times, *kanga* is used to wrap up like this. Most women wrap *kanga* like this when attending a burial or grieving someone who has passed away. Women wrap one *kanga* at the waist and, with another one, they cover themselves like this. You can also use *kanga* to cover yourself when you are in a hurry, like rushing to the market. One can just wrap one's *kanga* around her waist, and wear a shirt. Maybe she doesn't want to show some part of her body, so she just covers herself with *kanga*. Also, *kanga* is used to carry a baby on your back. This is how we carry a baby with *kanga*. Your baby is on your back, then this side of *kanga* is this way, and you tighten the *kanga* like this. So the baby will be in this position, and his legs hanging out this way. Again, you can cover your head with *kanga*. For example, in kitchen parties, they use *kanga* to dress the brides and they cover their heads with *kanga*. They can make a kind of flower like this, just a simple one, or like this. They can make any type of flower they wish, and this piece can be on this side, or at the back, or at the front. This is just an example. Other times, *kanga* can be used to decorate the house. They can tie like this, at the middle of the *kanga*, and make something like a butterfly and hang [it] on the wall. They can make this kind of decoration to decorate during a wedding, kitchen party or during Holy Communion. This is just an example, but if you make it good, it looks good on the wall -- like a butterfly.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.